# JARIDA LA RS RUVUMA

## TOLEO LA JANUARI 2025









## KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

**JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA JANUARI 2025**

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

# TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.
Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wa ngazi ya Wilaya,Mkoa na kitaifa wanavyofanya ziara za kuzungumza na wananchi,kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## SERIKALI YAKARABATI HOSPITALI YA TUNDURU ILIYOJENGWA MWAKA 1930



Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetoa fedha kwaajili ya kukarabati hospitali kongwe ya wilaya ya Tunduru iliyojengwa mwaka 1930.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Dr. Bernad Mwamanda, ameeleza kuwa wamefanikiwa kujenga jengo la wagonjwa wa nje (OPD) ambalo limegharimu milioni 900, na jengo la wagonjwa wa dharura (EMD) ambalo mwanzo halikuwepo limegharimu milioni 300.

Ameongeza kuwa majengo hayo yamekamilika, yanaendelea kutoa huduma na yana vifaa tiba ambavyo vinasaidia sana kwenye matukio ya dharura, pia wamepatiwa gari la kubebea wagonjwa ambapo awali walilazimika kuazima kutoka kituo kingine.

Mkazi wa Wilaya ya Tunduru, Sara Chifu, ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuboresha majengo ya hospitali na sasa ubora wa huduma zote ni mzuri na zinapatikana kwa wakati.

Kwa upande wake, mkazi mwingine wa wilaya hiyo, Juma Mahamba, amesema kuwa ukilinganisha awali na sasa, uboreshaji wa sasa umekuwa bora zaidi tofauti na awali.

## MRADI WA MAJI WA ZAIDI YA MILIONI 900 WAZINDULIWA NYASA



Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma umetambulisha mradi wa maji wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 962.7.

Mradi huu unalenga kutatua changamoto ya maji safi na salama katika vijiji vya Mbanga na Kigongo, kata ya Lumeme.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Mhe. Peres Magiri, amemtaka mkandarasi kuhakikisha mradi unajengwa kwa ubora na kukamilika kwa wakati. Amesisitiza kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha kila mwananchi anapata maji safi, hivyo fedha zilizotengwa ziendane na thamani halisi ya mradi.

Mradi huu unatarajiwa kuhudumia wananchi 4,990 kutoka vijiji vya Mbanga na Kigongo.

## CCM WATEMBELEA MRADI WA MAJI MIJI 28 SONGEA



CHAMA cha Mapinduzi wilaya ya Songea mkoani Ruvuma,kimempongeza Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa Sh.bilioni 145.77 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wa Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Pongezi hizo zimetolewa na Mwenyekiti wa Chama hicho Mwinyi Msolomi,wakati wa ziara ya wajumbe wa kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi Songea mjini

baada ya kutembelea mradi wa maji wa miji 28 unaotekelezwa na Mkandarasi kampuni ya China Civil Engineering Contruction Corporation(CCECC).

Mradi huo,unatarajiwa kumaliza kero ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Manispaa ya Songea hasa wanaoishi mtaa wa Sokoine kata ya Bombambili na Making'inda kata ya Msamala ambao mara kwa mara wanapata maji kwa mgao.

Msolomi,ameishukuru Serikali kupitia wizara ya maji na Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Manispaa ya Songea(Souwasa), kuanza kutekeleza mradi huo unaosubiriwa kwa hamu kubwa na wakazi wa Manispaa hiyo na maeneo mengine ya jirani.

Mjumbe wa Kamati hiyo Pascal Msigwa,amefurahishwa na maendeleo ya ujenzi wa mradi huo,lakini ameiomba Serikali kuharakikisha ujenzi wake ili wananchi waweze kupata huduma ya maji ya uhakika na kuwaondolea adha ya kupata huduma hiyo kwa mgao.

Msimamizi wa mradi huo kutoka Mamlaka ya maji na usafi wa mazingira Songea mjini(SOUWASA) Vicenti Bahemana alisema,mradi ulianza kutekelezwa mwezi Januari 2024 na unatarajia kukamilika mwezi Septemba 2026.



## MPANGO WA KUIBUA WAGONJWA WA KIFUA KIKUU WAZINDULIWA RUVUMA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amesema Ruvuma ni kati ya mikoa 9 iliyokuwa na uibuaji mdogo wa wagonjwa wa kifua kikuu kwa mwaka 2024 ambapo wagonjwa 1,278 waliibuliwa kati ya lengo la wagonjwa 2,515 waliopaswa kuibuliwa.

Ameyasema hayo wakati akizindua Mpango Harakishi wa Kuibua Wagonjwa wa Kifua Kikuu uliofanyika katika uwanja wa nje ya soko kuu la Songea mjini lililopo manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

"Kwa Mkoa wa Ruvuma wagonjwa walioibuliwa ni asilimia 50.79 tu, hivyo bado tunalo jukumu la kuwapata wagonjwa 1,132 ambao bado wapo katika jamii tunayoishi wakiendelea kuwaambukiza watu wengine," alisema Kanali Ahmed.

Ameongeza kuwa takwimu zinadhihirisha kuwa ugonjwa wa kifua kikuu ni janga kubwa na kikwazo kwa maendeleo ya Taifa kwa sababu wanaougua wanashindwa kuzalisha mali hivyo kutochangia vizuri katika pato la Taifa na kumudu maisha yao wenyewe.

Naye Mwakilishi kutoka Wizara ya Afya Dr. Jacob Mwanamtwa, amebainisha kuwa kampeni hiyo ilianza Januari 20, 2025 na hadi kufikia Januari 22 wamefanikiwa kukusanya sampuli kwa wagonjwa 851 na waliogundulika kuwa na ugonjwa huo na kuanza matibabu ni 24 sawa na asilimia 2.8.

Amelitaja lengo la kampeni hiyo ni uharakishaji wa uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu waliokosekana mwaka 2024 ili kuweka jitihada kwa pamoja na umoja katika kupambana na kifua kikuu, kuboresha na kuharakisha ufanisi wa huduma kwa wananchi.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Mhe. Kisare Makori, amesema kifua kikuu ni moja ya magonjwa yanayoambukizwa ambayo ni tishio hivyo wataendelea kushirikiana na viongozi mbalimbali wanaoratibu shughuli hiyo ili kuhakikisha zoezi hilo linafanikiwa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mhe. Kapenjama Ndile, amesema Tanzania ni moja kati ya nchi 30 zinazokabiliwa na tatizo la ugonjwa wa kifua kikuu hivyo amewashauru wananchi wa wilaya wa Songea kukata bima ya Afya ili ziwasaidie hata wanapopata tatizo la ugonjwa wa kifua kikuu wawe na uhakika wa kutibiwa.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2024 kulikuwa na wagonjwa milioni 10.8 wa kifua kikuu duniani kote, kati yao milioni 1.25 sawa na asilimia 12 walifariki kutokana na ugonjwa huo, Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa wapya laki 122,000 sawa na wagonjwa 183 kwa kila watu 100,000 walioibuliwa na kuanzishiwa dawa ni 92,720 sawa na asilimia 76.



## POLISI RUVUMA WAFANYA UKAGUZI WA VYOMBO VYA MOTO



Jeshi la Polisi Mkoa wa Ruvuma Kitengo cha Usalama Barabarani limefanya operesheni ya kushtukiza ya ukaguzi wa vyombo vya moto vya kusafirisha abiria na malori. Ukaguzi huo umebaini makosa kadhaa, yakiwemo magari mabovu, uchanganyaji wa mizigo na abiria, na madereva kuendesha magari huku leseni zao zikiwa zimeisha muda wa matumizi.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Ruvuma, Issa Milanzi, aliongoza operesheni hiyo akiwa ameambatana na waandishi wa habari. Ukaguzi ulifanyika katika stendi ya mabasi ya Seedfarm na eneo la Msamala.

“Gari haina honi, indiketa hazifanyi kazi, lakini dereva huyu anadiriki kusafirisha abiria. Pia kuna gari haina plate namba halali, badala yake imebadilishwa kinyume cha sheria,” alisema RTO Milanzi wakati wa ukaguzi

RTO Milanzi amewataka madereva wote mkoani Ruvuma kufuata sheria, kanuni, na taratibu za usalama barabarani ili kuepusha ajali zinazoweza kuzuilika. “Unapokwenda kinyume na sheria, unaweza kusababisha matatizo ambayo yangepaswa kuepukika kwa kufuata taratibu,” alisisitiza.

Madereva wa mabasi ya shule nao wamekumbushwa kufuata sheria ili kuhakikisha watoto wanafika salama shuleni na kurudi nyumbani bila ajali.

Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limejipanga kupunguza ajali

# DC NYASA AZINDUA KAMPENI YA UPANDAJI MITI



WILAYA ya Nyasa Mkoani Ruvuma imefanya uzinduzi wa siku ya upandaji miti kiwilaya katika Hospitali ya Wilaya ya Nyasa kwa kupanda miti katika eneo la hospitali na pembezoni mwa barabara za Kilosa.

Mgeni rasmi wa uzinduzi huo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Mhe. Peres Magiri, ambaye alihamasisha wananchi na watumishi kupanda miti 400 katika eneo la hospitali na miti 300 pembezoni mwa barabara ya Kilosa.

Mhe. Magiri aliwataka wananchi kupanda miti na kuitunza ili Wilaya ya Nyasa iwe eneo la kitalii kwa kuwa imepangwa vizuri. Alisisitiza umuhimu wa kupanda miti kama sehemu ya juhudi za kutekeleza agizo la serikali la kupanda miti milioni 1.5.

Amewaonya wafugaji wa mifugo dhidi ya kuachia mifugokudhurura na kuharibu miti iliyopandwa, akibainisha kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa watakaokiuka.

Naye Meneja wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Nyasa Elisha John,amesema wameandaa miche 30,000 ya miti kwa kila kata ili wananchi wapande na kuongeza kipato cha familia.

## MRADI WA MAJI NGUMBO WAPEWA PIKIPIKI MBILI



Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, mkoani Ruvuma Mhe. Peres Magiri, amekabidhi pikipiki mbili zilizonunuliwa na Serikali kupitia Mradi wa Maji wa Ngumbo awamu ya kwanza kwa vyombo viwili vya Watumia Maji: NGULIWSO cha Kata ya Ngumbo na Liwundi, na LILIMBAWSO cha Kata ya Lituhi, Linga, na Mbaha.

Makabidhiano hayo yalifanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, yakiwa yamehudhuriwa na wananchi, watumishi, na viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali.

Akikabidhi pikipiki hizo, Mhe. Magiri alimshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuipa Wilaya ya Nyasa pikipiki hizo pamoja na miradi ya maji ambayo imesaidia kutatua changamoto za wananchi. Aliwataka wanaopokea pikipiki hizo

kuzitunza na kuzitumia kwa manufaa ya jamii, hususan kutatua changamoto za maji.

“Ninawakabidhi pikipiki hizi zikatumike vizuri kutatua changamoto kwa wananchi, ikiwemo kutengeneza mabomba maji yanapokatika. Zisitumike kubebea abiria au kwa manufaa binafsi. Tukibaini matumizi mabaya, hatua kali za kisheria zitachukuliwa,” alisema Mhe. Magiri.

Kwa upande wake, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Nyasa Mhandisi Masoud Samila,, alisema kuwa pikipiki hizo zitasaidia kuongeza usimamizi wa miradi ya maji. Alibainisha kuwa Wilaya ina vyombo nane vya watumia maji, lakini vitano kati ya hivyo havina usafiri.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa, Mhandisi Stella Manyanya, ameipongeza Serikali kwa kuendelea kutatua changamoto za wananchi wa Jimbo la Nyasa.

## BILIONI 2.5 ZAJENGA SEKONDARI TANO ZA KISASA TUNDURU



Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi bilioni 2.5 kupitia mradi wa kuboresha miundombinu ya shule za sekondari (SEQUIP) kwaajili ya ujenzi wa shule 5 za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

Hayo yamebainishwa na Afisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mwalimu Rudia Elias Masatu, ambapo amesema fedha hizo zimetumika kujenga sekondari 5 ambazo ni Majimaji, Mpakate, Kungu, Tuwe Macho  na Tinginya ambazo tayari zina wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha tatu.

Naye Mwalimu Mkuu wa Kungu sekondari, Ayoub Kundya, amesema walipokea shilingi milioni 480 mwaka 2022 kwaajili ya ujenzi wa madarasa 8, jengo la utawala, maktaba, chumba cha kompyuta pamoja na maabara tatu za masomo ya Fizikia, Kemia na Biolojia, na shilingi milioni 95 kwaajili ya ujenzi wa nyumba za walimu ambazo zimekamilika, na shule hiyo tayari ina wanafunzi 467 wa kidato cha kwanza hadi cha tatu.

Kwa upande wake mwanafunzi wa kidato cha tatu wa Kungu sekondari, Frahma Seif Ali, ameishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kuwaletea shule nzuri na amehaidi wataongeza bidii ili kufanya vizuri kitaaluma.

Kwa upande mwingine Mjumbe wa Bodi ya Kungu sekondari, Mahmoud Selemani, amesema mwanzo wanafunzi walikuwa wanapata shida ya kutembea umbali mrefu hivyo shule hiyo imepunguza adha hiyo na sasa itawasaidia kupata masomo kwa wakati.

Katika hatua nyingine mzazi wa mwanafunzi anyesoma Kungu sekondari, Ahmad Mtumbi, amesema wamepata madarasa mazuri, shule ina muonekano mzuri na yenye mandhari mazuri.

## MUONEKANO WA SHAM,BA LA MITI WINO MADABA



Muonekano kutoka juu wa shamba la Miti Wino lililopo katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma

Hifadhi ya msitu wa Wino iliyopo katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma ni miongoni mwa mashamba 24 ya miti ya kupandwa yanayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

Hifadhi hii kwa sasa ina ukubwa wa hekta 39,718 zinazoundwa na safu tatu (Wino 2,259ha, Ifinga 29,000ha na Mkongotema 8,459ha).

Mhifadhi Mkuu wa Shamba miti Wino Glory Kasmiri anasema uhifadhi ya msitu wa Wino ulianza kuendelezwa na TFS mwaka 2010 ikihusisha eneo dogo la msitu wa asili wenye ukubwa wa hekta 2,259 (ambayo ndio safu ya Wino).





## WANAFUNZI 76,000 KUPEWA DAWA ZA MINYOO NA KICHOCHO



Wanafunzi 76,962 kutoka shule 102 katika Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma, wanatarajiwa kupatiwa dawa za kinga dhidi ya magonjwa ya minyoo ya tumbo na kichocho.

Zoezi hilo linafanyika kwa siku mbili, kuanzia tarehe Januari 23 hadi 24 2025, likiwalenga watoto wenye umri wa miaka mitano hadi 14.

Akizungumza kuhusu zoezi hilo, Mratibu wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele katika Manispaa hiyo, Dr.Bload Komba, amewahakikishia wazazi kuwa dawa hizo ni salama kwa matumizi na zinalenga kuimarisha afya ya watoto dhidi ya magonjwa hayo.



## UBORESHAJI DAFTARI LA WAPIGA KURA TUNDURU



UBORESHAJI wa daftari la kudumu la wapiga kura katika Jimbo la Tunduru Kusini na Kaskazini linatarajiwa kuanza tarehe 28 Januari 2025 hadi 3 Februari 2025. Wananchi wote wanahimizwa kushiriki kikamilifu kwani kujiandikisha ni msingi wa uchaguzi bora.

Mafunzo ya kina kwa waandishi wasaidizi wa ngazi ya kata (ARO-Kata) yamekamilika kwa mafanikio makubwa. Mafunzo haya yamewalenga kuwajengea uwezo wa kutekeleza zoezi la uboreshaji wa daftari kwa ufanisi na kuzingatia viwango vya ubora.

Mgeni rasmi katika hafla ya kufunga mafunzo hayo, Ndg. Chiza C. Marando, ametoa wito kwa watendaji kushirikiana kwa karibu ili kufanikisha zoezi hilo. Aidha, amesisitiza umuhimu wa kuchukua tahadhari za ziada kwa kuwa jimbo hilo linapakana na nchi jirani, kuhakikisha kuwa waliojiandikisha ni raia halali wa Tanzania.

“Taratibu zote zilizowekwa na Tume zinapaswa kufuatwa, na vifaa vyote vya zoezi hili kutunzwa kwa makini,” alisema Ndg. Marando, akihimiza mshikamano miongoni mwa watendaji.

# WANANCHI WAOMBA KUBORESHWA BUSTANI YA RUHILA




Wanchi wa wilaya ya Songea mkoani Ruvuma,wameishauri Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kuboresha Bustani ya wanyamapori Ruhila Zoo ili kushawishi na kuvutia watu wengi zaidi kwenda kutembelea bustani hiyo ya wanyama.

Wamesema,licha ya Mamlaka ya Udhibiti wa Wanyamapori Tanzania(Tawa) kanda ya Kusini kupeleka wanyama,lakini katika eneo hilo kuna changamoto nyingi ambazo serikali inatakiwa kuzifanyia kazi ili bustani ya wanyamapori Ruhila iwe chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali.

Aidan Komba,Mkazi wa mtaa wa Mshangano katika Manispaa ya Songea alisema,bustani ya Ruhila ikiboreshwa kwa kuwekwa miundombinu mizuri na rafiki kama maeneo mengi ya kucheza watoto,mabwawa ya kuogolea na kutembea kwa mitumbwi na wanyama wa kila aina itawashawishi watu wengi kutembelea tofauti na ilivyo sasa.

Agostino Nombo,ameiomba Serikali kutupia jicho bustani ya wanyamapori Ruhila kwa kuweka mazingira mazuri ili kuwavutia watu kwenda kuona vivutio mbalimbali

vilivyopo kama vile wanyama,ndege na miti aina mbalimbali iliyozunguka kwenye bustani hiyo iliyoanzishwa tangu mwaka 1973.

Helen Kavishe,ameipongeza TAWA kwa kuleta wanyama mbalimbali katika Bustani ya Ruhila Zoo ambapo alieleza kuwa, sasa wananchi wa Ruvuma hususani wanaoishi katika manispaa ya Songea wamepata sehemu nzuri ya mapumziko na kuwataka wananchi wenzake kuhakikisha wanakwenda kutembelea bustani hiyo ili waweze kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vilivyopo.

Serikali kupitia mamlaka ya usimamizi Wanyamapori Tanzania(TAWA) chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii imeleta Simba wawili majike waliopewa majina ya Lucy na Liana katika Bustani hiyo kutoka Hifadhi ya Wanyamapori ya Seva jijini Arusha ili kuchochea utalii wa ndani.

Bustani hiyo imeanzishwa kwa ajili ya wananchi wa mkoa wa Ruvuma na Watanzania kwa ujumla, kama mkakati wa Serikali ya mkoa wa Ruvuma katika kumuunga mkono Rais Dkt Samia Suluhu Hassan katika kuboresha sekta ya utalii

Bustani ya Wanyamapori Ruhila iliyopo katika Manispaa ya Songea ina wanyama wa aina mbalimbali kama vile Pofu,nyumbu Pundamilia, kakakuona, sungura, nyani,kuro na swalapala.



# WAKULIMA TUNDURU WAUZA KILO MILIONI 19 ZA KOROSHO



KILO milioni 19,375,896.00 za korosho zenye thamani ya Sh.bilioni 62,159,126,758.00 zimeuzwa na wakulima wanaohudumiwa na Chama kikuu cha Ushirika wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma(TAMCU Ltd).

Korosho hizo zimeuzwa katika minada minne kupitia mfumo wa stakabidhi ghalani chini ya usimamizi wa mfumo soko la bidhaa(TMX) ulioonyesha mafanikio makubwa kwa wakulima kupata soko la uhakika na bei nzuri ya zao hilo.

Meneja Mkuu wa TAMCU Marcelino Mrope alisema,mnada wa kwanza ulifanyika katika kijiji cha Nakapanya kilo 1,804,369.00 zenye thamani ya Sh.5,792,024,490.00 zimeuzwa kwa bei ya Sh. 3,210 kwa kilo moja.

Mrope alisema,katika mnada wa pili uliofanyika katika kijiji cha Mtina wakulima wameuza kilo 7,543,517.00 zenye thamani ya Sh.23,973,297,026.00 kwa bei ya Sh. 3,178.

Kwa mujibu wa Mrope,mnada wa tatu uliofanyika kijiji cha Airpot kata ya Mbesa, kilo 5,190,191.00 zimeuzwa kwa bei ya Sh.3,212 huku wakulima wakipata zaidi ya Sh. 16,670,893,492.00 na katika mnada wanne uliofanyika tarehe 12 Novemba kijiji cha Ligoma kilo 4,837,819.00 zenye thamani ya Sh.15,722,911,750.00 ziliuzwa kwa bei ya Sh.3,250.

.

# MAANDAMANO YA CCM NYASA KUMUUNGA MKONO RAIS SAMIA



Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma wamefanya maandamano ya kumpongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa mgombea urais mwaka 2025 kupitia CCM, pamoja na kumshukuru kwa kumteua Dkt. Emmanuely Nchimbi kuwa mgombea mwenza.

Maandamano hayo yaliandaliwa kuunga mkono maazimio ya Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma, ambapo wajumbe walimchagua Dkt. Samia kuwa mgombea urais wa Tanzania Bara, Dkt. Nchimbi kuwa mgombea mwenza, na Dkt. Hussein Mwinyi kuwa mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Akizungumza wakati wa kufunga maandamano hayo, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM Wilaya ya Nyasa, Komredi Clavian Matembo, alisema wamefurahishwa na maamuzi ya chama na wanaunga mkono uteuzi wa Dkt. Samia na Dkt. Nchimbi. Alisema, “Tunaamini maazimio haya ni ya busara, na Umoja wa Vijana wa Nyasa tuko pamoja na chama chetu katika safari hii.”

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa CCM Tanzania Bara, CDE Mussa Mwakitinya, aliwapongeza vijana wa Nyasa kwa kuandaa maandamano ya amani kama ishara ya kuunga mkono maamuzi ya chama.

## BODI YA USHAURI YA RRH RUVUMA YAZINDULIWA



Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan imefanya maboresho makubwa ya huduma za afya katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma.

Akizungumza kwenye ufunguzi na uzinduzi wa Bodi mpya ya Ushauri ya hospitali hiyo mjini Songea Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Songea Dr.Magafu Majura amesema Katika kipindi cha 2020-2024, serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 8.6 kwa ujenzi wa majengo na ununuzi wa vifaa tiba.

Ameitaja Miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kuwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje,OPD, wodi ya wagonjwa wa dharura , na jengo la mionzi ambalo limeanza kutumika.

“Maboresho ya hospitali yameongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa kiasi kikubwa,Changamoto kuu zinazoikabili hospitali ni pamoja na upungufu wa watumishi kwa asilimia 25,Ukosefu wa baadhi ya dawa ,vifaa tiba na Miundombinu dhaifu katika baadhi ya maeneo”,alisema Majura.

Kwa upande wake mgeni rasmi katika hafla hiyo Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed aliyewakilishwa na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea Mheshimiwa Michael Mbano amesema lBodi mpya imepewa jukumu la

kusimamia huduma bora kwa wananchi, kuimarisha uwajibikaji wa watendaji, na kushughulikia changamoto zilizopo. Hata hivyo amesema Serikali itaendelea kutoa msaada wa rasilimali, mafunzo, na miongozo ili kuhakikisha mafanikio ya bodi.

Ametoa rai kwa Mwenyekiti wa Bodi mpya pamoja na wajumbe kuhakikisha mipango ya maendeleo inatekelezwa kwa kuzingatia sheria, kanuni, na taratibu.

Bodi mpya ya Ushauri ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma, iliyozinduliwa rasmi,iliundwa Oktoba 8, 2024, unatarajia kumaliza muda wake Septemba 4, 2027.

## WALIMU 128 NYASA WAPATA MAFUNZO KUBORESHA ELIMU



Ofisi ya Rais TAMISEMI, kupitia Mradi wa BOOST, imetoa mafunzo kwa walimu wakuu 64 na walimu wanaofundisha shule za awali katika shule za msingi 64, jumla ikiwa walimu 128. Mafunzo hayo yanalenga kuboresha elimu ya awali kwa kuhakikisha wanafunzi wanajua kusoma, kuandika, na kuhesabu.

Mafunzo hayo yamefanyika katika Shule ya Msingi Nyasa, iliyopo katika kijiji cha Kilosa, kata ya Kilosa, wilayani Nyasa.

Mratibu wa mafunzo hayo, Mwalimu Godfried Mapunda, amesema lengo kuu ni kuwajengea uwezo walimu ili waweze kufundisha wanafunzi kwa ufanisi zaidi kwa kutumia zana bora za kujifunzia. Hii itasaidia wanafunzi kupenda shule na kupata maarifa ya msingi kwa ubora.

**SEKONDARI YA SAMIA ILIVYOWAKOMBOA WATOTO WA KIKE**




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amefungua rasmi shule ya mfano ya wasichana katika Mkoa wa Ruvuma, wilayani Namtumbo. Shule hiyo imegharimu shilingi bilioni 4.35 kukamilika.

Makamu Mkuu wa shule, Bw. Bernad Komba, amesema ujenzi wa shule umejumuisha jengo la utawala moja (1), madarasa ishirini na mawili (22), bwalo moja la chakula (1), mabweni tisa (9) kwa wanafunzi, maabara nne (4), maktaba, na chumba cha TEHAMA. Shule hiyo ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200, lakini kwa sasa ina wanafunzi 548 kutoka kidato cha kwanza, cha tano, na cha sita.

Kufikia Januari mwaka huu, shule hiyo inatarajia kupokea wanafunzi 128 wa kidato cha kwanza, na hivyo kuongeza idadi ya wanafunzi kufikia 700.

Mwanafunzi Groli Gama amepongeza jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwajengea shule yenye mazingira rafiki na wezeshi, yanayowapa nafasi wanafunzi wa kike, wakiwemo wenye ulemavu, kujifunza bila changamoto yoyote.

Shule hii imekuwa mfano wa kuigwa kwa kuboresha mazingira ya elimu kwa wasichana, ikiwa ni sehemu ya juhudi za serikali kuinua sekta ya elimu nchini.

## MWENYEKITI WA TUME HURU YA UCHAGUZI AMTEMBELEA RC




Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele akiambatana na Katibu wa Tume ambaye pia ni Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume, Bw. Kailima Ramadhani leo Januari 03, 2025 wamemtembelea ofisini kwake, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ambapo pamoja na mambo mengine walimpa taarifa ya uwepo wa zoezi la uboreshaji wa daftari la Kudumu la Mpiga Kura Januari 12 hadi 18, 2025 na Januari 28 hadi Februari 3,2025 katika mkoa wa Ruvuma



.

## RC AWAONGOZA KUWAAGA WALIPOTEZA MAISHA KWA AJALI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amewaongoza wananchi kuaga miili ya watu sita waliopoteza maisha kwenye ajali ya gari iliyotokea katika kijiji cha Chunya Wilayani Mbinga.

Tukio hilo limefanyika katika uwanja wa michezo wa CCM uliopo Halmashauri ya Mji wa Mbinga na kukabidhi miili hiyo kwa ndugu wa marehemu kwaajili ya kufanya maziko.

Akitoa salamu za pole wakati wa kuaga miili hiyo, Kanali Ahmed, amesema hiki ni kipindi kigumu na kinachoumiza hasa unapoangalia aina ya kifo kilichotokea, amewapa pole waliowapoteza wapendwa wao na kuwasihi watu wote kutumia msiba huo kutafakari maneno ya viongozi wa dini, kujiandaa kwa kusali, kufanya toba, na kushiriki kwenye matukio kama hayo kwa kuwa hakuna ajuaye siku wala saa.

"Kuagana kwa aina hii hakuleti faraja hata siku moja, unaagana na mtu ambaye huwezi tena kukutana naye, ni kipindi kigumu, ni kipindi kinaumiza, kinaumiza zaidi unapoangalia aina ya kifo kilivyotokea, ndugu zetu hawa hawakuwa hata na dakika moja ya kujitetea, baadhi yao ni vijana wadogo walikuwa wana ndoto zao binafsi lakini Taifa lilikuwa lina ndoto kubwa dhidi yao, nimeyapokea haya kwa maumivu

makubwa sana, na kwa idadi hii Mkoa na Taifa limepoteza nguvu kazi," alisema Kanali Ahmed.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Bi. Mary Makondo, amesema kutokana na ajali hiyo Shule ya Msingi Lumalu iliyokuwa na walimu watano imepoteza walimu wanne, hivyo watalifanyia kazi swala hilo ili wapate walimu wengine kwaajili ya kuendelea kutoa huduma shuleni hapo.

Kwa upande mwingine Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Ruvuma, Komred Oddo Mwisho, amesema wananchi sita kuondoka kwa wakati mmoja ni idadi kubwa sana wakati bado walikuwa wanahitajika kulitumikia Taifa, hivyo Chama cha Mapinduzi kimepokea kwa masikitiko makubwa kwa kuondokewa na nguvu kazi kubwa na aina ya kifo kilichowapata.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Mhe. Kisare Makori amesema anaweza kuhisi maumivu wanayopata wafiwa Kwa kuwa wapo waliopoteza wazazi, watoto na wengine wake, amesema neno la Mungu likawape faraja wafiwa hao katika kipindi kigumu wanachopitia.

Ajali hiyo iliyosababisha vifo vya watu sita ilitokea Disemba 28, 2024 katika kijiji cha Chunya wilayani Mbinga ilihusisha gari ndogo aina ya Prado ( T 647 CVR ) baada ya kupinduka na kuwaka moto, waliopoteza maisha ni walimu wanne wa shule ya msingi Lumalu ambao ni Damas Damasi Nambombe, Dominika Abehart Ndau, Judith Joseph Nyoni na John Silvester Mtuhi, dereva wa gari hiyo Vincent Alex Milinga pamoja na Raia mmoja Bonface Bosco Mapunda.



## CCM RUVUMA  KUPANDA MITI KWENYE MAADHIMISHO YA CCM




Katibu  wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa Ruvuma Ndugu Mohamed Ally amesema chama hicho kimedhamiria kuendeleza kampeni ya upandaji miti kwenye maadhimisho ya kuzaliwa  CCM mwaka huu hiyyo amewaomba Wakala wa Misitu  Tanzania TFS kuwaandalia miche ya kutosha ili kutekeleza mpango huo utakaosaidia kulinda na kuhifadhi mazingira ya Mkoa wa Ruvuma.

Mohomed ametoa ombi hilo mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakati anazungumza kwenye uzinduzi wa upandaji miti ngazi ya Mkoa wa Ruvuma katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea ambapo Kanali Abbas amewaagiza TFS kuhakikjsha wanaandaa miche ya kutosha kufanikisha zoezi hilo ikiwa ni muendelezo wa kampeni za upandaji miti mkoani Ruvuma



## UZINDUZI UPANDAJI MITI MKOANI RUVUMA



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo akipanda mti kwenye uzinduzi wa upandaji miti ngazi ya Mkoa wa Ruvuma katika viwanja wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea eneo ;a Mwengemshindo Manispaa ya Songea ,ambapo mgeni rasmi kwenye uzinduzi huo alikuwa ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma Ndugu Mohamed Ally akipanda mti kwenye viunga vya kituo cha Afya Kata ya Ruvuma Manispaa ya Songea kwenye uzinduzi wa upandaji miti ngazi ya Mkoa wa Ruvuma ambapo Mkoa umedhamiria kupanda miti zaidi ya milioni sita

## KAMPENI ZA UPANDAJI MITI MKOANI RUVUMA



Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akipanda mti kwenye viunga vya hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea eneo la Mwengemshindo Manispaa ya Songea ambako ulifanyika uzinduzi wa upandaji miti ngazi ya Mkoa wa Ruvuma . Msimu huu Mkoa wa Ruvuma unatarajia kupanda miti zaidi ya milioni sitakatika Halmashauri zote nane lengo ni kundelea kuufanya Mkoa wa Ruvuma unakuwa wa kijani na kulinda mazingira kwa ustawi wa kizazii cha sasa na kijacho.



# RC RUVUMA ATEMBELEA BUSTANI YA MITI MATOGORO



Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akitembelea bustani ya miche ya miti Hifadhi ya Matogoro Manispaa ya Songea pamoja na vivutio vya utalii vilivyopo katika hifadhi hiyo ikiwa ni sehemu ya uzinduzi wa upandaji miti ngazi ya Mkoa wa Ruvuma ambapo Mkoa umedhamiria kupanda miti zaidi ya milioni sita msimu huu ili kuendelea kuufanya Mkoa kuwa wa kijani na kulinda mazingira na vyanzo vya maji



# SOTE TUSHIRIKI UTUNZAJI WA MAZINGIRA-RAS RUVUMA



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo akizungumza kwenye uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti ngazi ya Mkoa wa Ruvuma uliofanyika katika viunga vya hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea eneo la Mwengemshindo Manispaa ya Songea ambapo pamoja na mambo mengine amesisitiza wananchi wote kujitokeza kupanda miti ili kuhifadhi na kulinda mazingira ya Mkoa wa Ruvuma



## RC RUVUMA ABORESHA TAARIFA ZAKE



Pichani Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, akiboresha taarifa zake katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Ofisi ya Mtaa wa Mashujaa Kata ya Mjini iliyopo Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Zoezi hili lililoanza Januari 12, linatarajiwa kukamilika Januari 18, 2025, katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Halmashauri ya Mji Mbinga, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, na Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa.

## NDC WAFANYA ZIARA YA MAFUNZO RUVUMA




Pichani ni wakufunzi na wanachuo wapatao 29 kutoka Chuo cha Taifa cha Ulinzi,National Defense College (NDC ) wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ofisini kwake mjini Songea.

# HALMASHAURI YA SONGEA YAZINDUA UPANDAJI MITI




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amezindua kampeni ya upandaji wa miti katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambayo imefanyika katika shamba la kampuni ya Aviv Tanzania Limited inayojishushulisha na kilimo cha kahawa mkoani Ruvuma.

Kampeni hiyo iliyoandaliwa na kampuni ya Aviv kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ili kuunga mkono juhudi za Serikali za kutunza mazingira imezinduliwa kwa kupanda miti pembezoni mwa milima ya Litenga katika shamba la kahawa la Aviv lililopo Lipokela Wilayani Songea mkoani Ruvuma.

Kabla ya uzinduzi huo Kanali Ahmed, amewasisitiza wananchi kuendelea kutunza mazingira kwa kupanda miti na kuitunza ili iweze kukua na kuona matokeo ya upandaji huo, pia ameipongeza Aviv Tanzania Limited kwa kuzingatia sheria za nchi na kimataifa kwa kupanda miti.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Mary Makondo, amesema wataendelea kushirikiana ili zoezi hilo liwe endelevu kwa kuhimizana kupanda miti mingi na kuitunza ili kuhakikisha mazingira yanaendelea kuboreshwa na isaidie kuleta mvua nyingi zaidi.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mhe. Kapenjama Ndile, amebainisha kuwa Aviv imetoa miche laki moja kwaajili ya kupanda katika mashamba ya kahawa, pia amewasisitiza wakulima wa kahawa kutokata miti ya asili ili kupanda kahawa badala yake wanatakiwa kupanda miti mingine ili kutunza mazingira na kupata soko la zao hilo kutokana na sera za kimataifa.

Kwa upande mwingine Meneja wa Aviv Tanzania Limited, Hamza Kassim, amesema Aviv ipo pamoja na Serikali na sera ya Umoja wa Mtaifa katika kuhakikisha suala la mazingira linakuwa namba moja kwa kuwaelimisha wananchi maana ya uhifadhi wa mazingira ili nchi isigeuke jangwa

## RC RUVUMA AAGIZA WANAFUNZI WOTE KURIPOTI SHULE



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amewataka wasimamizi wa elimu ngazi ya mkoa, wilaya na halmashauri kuhakikisha watoto wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa na waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaripoti shuleni.

Ameyasema hayo wakati akifanya mkutano na waandishi wa habari kuhusu mwaka mpya wa masomo, uliofanyika katika ofisi yake iliyopo mjini Songea mkoani Ruvuma.

"Tuendeleze kasi na nguvu ya kusimamia zoezi hili ili liwe na mafanikio makubwa, kila mtoto anayestahili kandikishwa awe ameandikishwa, wanafunzi wote

waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wahakikishe wote wanaripoti shule, viongozi waliopo katika mamlaka ya ngazi za wilaya na halmashauri wahakikishe wanaendelea kusimamia zoezi hilo ili wale ambao wanakiuka sheria wachukuliwe hatua,"alisema Kanali Ahmed.

Ameongeza kuwa zoezi hilo liende sawa na kuhakikisha wazazi wanawapatia watoto wao mahitaji stahiki ikiwemo sare za shule, shajara na kuhakikisha mtoto anapata chakula shuleni ili kumpunguzia vikwazo katika masomo yake.

Amemsisitiza kila mdau anayehusika na ujenzi wa miundombinu ya shule kuhakikisha anatimiza wajibu wake, miradi ya ujenzi inayojegwa izingatie ufanisi pamoja na kukamilishwa mapema ili wanafunzi waweze kuitumia miundombinu hiyo.

Kwa upande mwingine ameiagiza Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa na Halmashauri kuchukua hatua za kinidhamu kwa mtu yoyote anayerudisha nyuma usimamizi wa elimu katika mkoa, hivyo kusiwe na vikwazo vyovyote vya kumpokea wanafunzi shuleni kwa kisingizio chochote cha mzazi kutotimiza mahitaji ya shule kwa sababu ni muhimu kila mwanafunzi kuanza masomo na wenzake kwa wakati.



***Muonekano wa sasa wa sekondari maalum ya wasichana ya Mkoa wa Ruvuma iliyojengwa wilayani Namtumbo ambayo imepewa jina la Dkt.Samia Suluhu Hassan***

## DC SONGEA AAGIZA KUBORESHA STENDI YA RUHUWIKO



Mkuu wa Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma Mheshimiwa Kapenjama Ndile, ametoa maelekezo kwa wataalamu wa Manispaa ya Songea kuhakikisha wanaboresha miundombinu ya stendi ndogo ya Ruhuwiko ili kuimarisha huduma kwa wananchi.

Ndile ametoa agizo hilo wakati wa ziara ya kushitukiza katika eneo hilo, ambapo alibaini changamoto kadhaa zinazohitaji kutatuliwa haraka.

Changamoto hizo ni pamoja na ukarabati wa choo cha kulipia kinachosimamiwa na Halmashauri, ujenzi wa kibanda cha kukaa abiria wakati wanasubiri usafiri, na ukosefu wa maji safi katika eneo hilo.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo, Ndile ameagiza changamoto hizo zitatuliwe ndani ya muda wa wiki moja.

Katika ziara hiyo Mkuu wa Wilaya aliongozana na wataalamu wa Manispaa ya Songea

Ziara hiyo inatarajiwa kuchochea maboresho ya haraka katika stendi ya Ruhuwiko ili kuboresha huduma kwa wananchi na kuongeza ufanisi wa miundombinu.

## TUNDURU WALIVYODHAMIRIA KUONGEZA UZALISHAJI KOROSHO



Vijana, maafisa ugani 50 wameanza kupatiwa mafunzo ya siku tano ya kuwajengea uwezo katika kukuza uzalishaji wa zao la korosho Wilayani Tunduru mkoani Ruvuma

Mafunzo hayo yanayoratibiwa na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Kupitia Mpango wa Jenga kesho iliyo bora (BBT), uliopo wizara ya Kilimo, yanalenga kuwajengea vijana hawa uwezo wa vitendo ili waweze kumsaidia Mkulima wa zao la Korosho kuongeza tija katika uzalishaji wa zao hilo.

Maafisa Ugani hao ni sehemu ya Maafisa Ugani na kilimo 500 katika mpango jenga kesho iliyo bora (BBT), Uliopo Wizara ya Kilimo, ambao wamesambazwa katika Mikoa ya Mtwara,Lindi,Ruvuma na Pwani.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Ndg. Milongo Sanga Katibu Tawala Wilaya ya Tunduru, amewasisitiza vijana hao kutimiza majukumu yao kwa dhati ili kuhakikisha lengo la Taifa la kufikia uzalishaji wa zao la Korosho tani 700,000 ifikapo mwaka 2025/2026 na tani 1,000,000 ifikapo 2029/2030.

## WALIMU WAPELEKWA LUMALU KUTEKELEZA AGIZO LA RC



Agizo la Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, limetekelezwa kwa mafanikio baada ya walimu watano kuhamishiwa Shule ya Msingi Lumalu, iliyoko Kata ya Upolo, wilayani Nyasa.

Hatua hii imechukuliwa kufuatia ajali ya gari iliyotokea tarehe 28 Desemba 2024 katika eneo la Burma, wilayani Mbinga, ambapo walimu wanne wa shule hiyo walipoteza maisha.

Afisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Mwalimu Benjamin Kusaga, amewaongoza walimu hao wapya hadi shuleni Lumalu, ambayo ina jumla ya wanafunzi 424 wanaosoma kuanzia darasa la kwanza hadi la saba.

Pichani, Mwl. Kusaga (wa tatu kutoka kushoto) akiwa na walimu hao watano waliopangiwa kazini, hatua inayolenga kurejesha hali ya kawaida ya masomo shuleni hapo.

# HALMASHAURI YA MBINGA KUJENGA HOSTELI YA HOSPITALI



Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma imekuja na mkakati wa ujenzi wa hosteli katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambayo itatoa huduma kwa wananchi ambao wamewaleta ndugu zao kuja kupata huduma za afya katika hospitali hiyo.

Utekelezaji huo ni chanzo cha mapato ya ndani ya Halmashauri utaondoa adha kwa wananchi ambao wanalazimika kutafuta malazi maeneo mbalimbali ambayo yapo mbali na hospitali hiyo.

Mkakati huo umebainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura katika ziara yake ya kutembelea Hospitali hiyo kukagua utoaji wa huduma za afya pamoja na ujenzi wa wodi tatu unaoendelea kutekelezwa.

## AWAMU YA PILI UBORESHAJI DAFTARI KUANZA RUVUMA




Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imezindua mafunzo kwa watendaji ngazi ya mkoa kuhusu Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya pili ambayo itajumuisha Halmashauri tatu za mkoa wa Ruvuma ambazo ni Tunduru DC, Namtumbo DC na Madaba DC.

Uzinduzi huo umefanyika katika ukumbi wa Chandamali mjini Songea mkoani Ruvuma, mgeni rasmi akiwa ni Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Mhe. Magdalena K. Rwebangira.

Mheshimiwa Rwebangira amewataka watendaji hao hasa wale waliowahi kufanya zoezi kama hilo kutumia uzoefu walionao na mafunzo wanayopatiwa kwa kufanya kazi zao kwa weledi, bidii na moyo wa kujituma ili kufanikisha zoezi hilo.

Ameongeza kuwa wakati wa Uboreshaji wa Daftari mawakala wa vyama vya siasa wataruhusiwa kuwepo katika vituo vya uandikishaji kwa kuwa ni muhimu na itasaidia kuleta uwazi katika zoezi zima na kutambua waombaji wa eneo husika hivyo kupunguza kutokea vurugu zisizo za lazima.

Naye Mratibu wa Uandikishaji Mkoa wa Ruvuma, Salumu Kateula, amebainisha kuwa awamu ya kwanza ya Uboreshaji wa Daftari ambayo ilianza tarehe 12 Januari inatarajia kukamilika Januari 18 ambayo imejumuisha Halmashauri tano katika mkoa linaendelea vizuri, na awamu ya pili ambayo itajumuisha Tunduru DC, Namtumbo DC na Madaba DC itaanza Januari 28 hadi Februari 3, 2025.

Amewasisitiza wananchi wa Halmashauri hizo kutumia muda huo kujitokeza kujiandikisha na kuboresha taarifa zao katika Daftari ili waweze kupata haki yao ya kupiga kura katika uchaguzi ujao.

Kwa upande wake Afisa Muandikishaji Jimbo la Madaba, Sajidu Mohammed, amesema wanaendelea kuwahamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha na kuboresha taarifa zao hasa makundi ya vijana waliotimiza umri wa miaka 18 na watu wenye ulemavu.

Awamu ya kwanza ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mkoani Ruvuma lilianza Januari 12 na linatarajiwa kukamilika Januari 18 katika Halmashauri tano ikiwemo Songea MC, Songea DC, Mbinga TC, Mbinga DC na Nyasa DC na awamu ya pili itaanza Januari 28 na kukamilika Februari 3 mwaka huu.




Idadi ya vijiji vya Mkoa wa Ruvuma vinavyopata umeme vimeongezeka hadi kufikia 489 sawa na asilimia 88.3 ya vijiji vyote 554 vya Mkoa wa Ruvuma.

# RAIS SAMIA ATOA MATREKTA MATATU NAMTUMBO




Wakulima wa Wilaya ya Namtumbo wamempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kugawa matrekta matatu ambayo yameanza kunufaisha wakulima wa tarafa tatu za wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Mhe. Ngollo Malenya, amewataka wakulima kutumia matrekta hayo kwa ufanisi ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati kama mbaazi, ufuta, soya, na mazao mengine ya kibiashara.



.

## DC SONGEA AHIMIZA KILIMO CHA NGANO



Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mheshimiwa Kapenjama Ndile, amewahimiza wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kuanza kulima zao la ngano, akisisitiza kuwa soko tayari lipo kupitia kampuni ya bia ya Serengeti.

Akizungumza na wananchi, Ndile alisema ofisi yake imefanya mazungumzo na kampuni hiyo, ambayo imekubali kununua ngano mara baada ya mavuno.

Aliahidi kutoa mbegu bure kwa wakulima wenye mashamba ya hekari moja au zaidi, huku akisisitiza juhudi za kuwawezesha kupata mbolea.

“Mwaka huu nimebuni mpango huu, na nyie mnatakiwa kuniunga mkono. Tutawapeni mbegu bure, na kampuni ya Serengeti tayari imekubali kununua mazao yenu,” alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mheshimiwa Teofanes Mlelwa, amempongeza Mkuu wa Wilaya kwa juhudi zake, akibainisha kuwa miaka 30 iliyopita wananchi wa eneo hilo walikuwa wakilima ngano lakini walikata tamaa kutokana na kukosekana kwa soko.

“Kwa maelekezo mazuri ya Mkuu wa Wilaya, kwamba ataleta mbegu na wanunuzi wa zao la ngano, tunaomba mpango huu utekelezwe haraka ili wananchi waweze kulima kwa wakati,” alisema Mlelwa.

Wananchi wamehimizwa kuchangamkia fursa hiyo ili kuboresha maisha yao na kuchangia maendeleo ya kilimo katika wilaya hiyo.

## KLINIKI YA SAMIA YASIKILIZA KERO ZA WALIMU 1,000 RUVUMA




Walimu 1,000 wa shule za msingi na sekondari mkoani Ruvuma wamejitokeza kuwasilisha kero zao wa wajumbe wa Kliniki Maalum ya kushughulikia kero za walimu (Samia Teachers Clinic) kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Walimu hao wamejitokeza kwenye ukumbi wa Kanisa Anglikana Dayosisi ya Ruvuma mjini Songea katika Timu ya Samia Teachers Clinic ambayo imeanzishwa kwa lengo la kusikiliza na kutatua changamoto za walimu kote nchini.

Akizungumza kwenye kikao hicho ambacho kiliwakutanisha walimu Zaidi ya 1,000 kutoka Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma,Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Ndugu Mary Makondo amewapongeza walimu waliojitokeza kuwasilisha kero zao.

“Walimu wengi wamefikiwa na maafisa waandamizi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI wakiwa na laptop kwa ajili ya kutatua kero zao kwenye mifumo’’,alisema Makondo.

Kwa upande wake Afisa Elimu Mkoa wa Ruvuma Mwl. Edith Mpenzile amesema walimu wamekuwa wanakabiliwa na kero mbalimbali hivyo kitendo hicho kinawatia moyo walimu na kuwa na ari katika uwajibikaji wanapokuwa darasani.


Naye Makamu wa Rais wa CWT Taifa Mwl. Suleiman Ikomba amezitaja baadhi ya changamoto zinazowakabili walimu nchini kuwa ni miundo ya utumishi wa walimu,madaraja ya mseleleko,kucheleweshwa kupandishwa madaraja na madai ya mapunjo mbalimbali ya mishahara



Muonekano wa hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea iliyojengwa katika Kijiji cha Mpitimbi ambayo imekuwa mkombozi wa wananchi wa Jimbo la Peramiho



## DC AWASHUKURU WANANCHI USHIRIKIANO KWENYE MAAFA



Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mheshimiwa Kapenjama Ndile, amewashukuru wananchi na wadau mbalimbali kwa kushirikiana katika kuwasaidia waathirika wa maafa yaliyosababisha uharibifu mkubwa wa nyumba na chakula.

Mheshimiwa Ndile alisema kuwa jumla ya nyumba 1,155 ziliharibika kutokana na mvua kubwa zilizonyesha hivi karibuni.

Katika tathmini ya uharibifu, nyumba 16 zimeharibiwa katika kijiji cha Madaba, nyumba 7 katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, na nyumba 133 katika Manispaa ya Songea. Aidha, Mheshimiwa Ndile alieleza kuwa hali hiyo imesababisha hasara kubwa kwa familia nyingi, huku baadhi ya nyumba zikishindwa kuhimili mvua kali.

Mkuu wa Wilaya amesisitiza umuhimu wa ushirikiano katika kusaidia waathirika wa maafa hayo, akisema kuwa msaada kutoka kwa wananchi na wadau umefanikisha mchakato wa kurejesha hali ya kawaida kwa baadhi ya familia zilizoharibiwa nyumba zao. Hata hivyo, ametoa wito kwa serikali na mashirika ya kutoa misaada kuongeza juhudi ili kuharakisha mchakato wa ujenzi wa nyumba na usambazaji wa chakula kwa familia zilizoathirika.



Pichani katikati mwenye kilemba ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo akiwa na Timu ya wajumbe wa Kliniki Maalum ya kushughulikia kero za walimu

WALIMU 1,000 wa shule za msingi na sekondari mkoani Ruvuma wamejitokeza kuwasilisha kero zao wa wajumbe wa Kliniki Maalum ya kushughulikia kero za walimu (Samia Teachers Clinic) kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI.

## DC MBINGA AZINDUA KAMPENI YA UPANDAJI MITI



Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, mkoani Ruvuma Mhe. Kisare Matiku Makori, amezindua rasmi kampeni ya upandaji miti katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga, hafla iliyofanyika katika Shule ya Msingi Lusonga.

Kampeni hiyo, iliyoandaliwa na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kwa kushirikiana na Kitengo cha Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira cha Halmashauri ya Mji wa Mbinga, inalenga kuunga mkono jitihada za serikali za utunzaji wa mazingira.

Akihutubia katika uzinduzi huo, Mhe. Makori alisisitiza umuhimu wa upandaji miti kama njia ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Pia alihimiza wananchi kuachana na tabia hatarishi kwa mazingira, kama uchomaji miti na matumizi ya mkaa, na badala yake kutumia nishati safi ya kupikia.

“Wale wenye utaratibu wa kuhujumu mazingira kwa kufanya vitendo vilivyokatazwa kisheria wanapaswa kubadilika ili tushirikiane kutunza mazingira,” alisema Mhe. Makori.

## STOF YATATUA CHANGAMOTO ZA MAJI SONGEA



TAASISI ya Isiyokuwa ya Kiserikali ya St.Teresa Orphans Foundation (STOF) imetoa Zaidi ya shilingi milioni 30 kukarabati majengo ,kununua madawati 25,kukarabati na kuchimba visima vitatu katika shule za msingi tatu Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Hayo yamesema na Mkurugenzi wa STOF nchini Tanzania Moses Nyirenda katika hafla ya kuishukuru STOF iliyofanyika katika shule ya msingi Unangwa ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Mkurugenzi wa STOF nchini Marekani Teresa Nyirenda.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa STOF nchini Tanzania,kati ya fedha hizo,jumla ya shilingi milioni 15 zimetolewa kwa ajili ya kukarabati majengo ya shule ya msingi Unangwa, shilingi 700,000 zimetumika kununua madawati 25 katika shule hiyo na shilingi 600,000 zimetumika kukarabati kisima cha maji.

Nyirenda amebainisha Zaidi kuwa STOF pia imetoa shilingi milioni 15.9 kuchimba visima viwili vya maji katika shule za msingi Msamala na Mkuzo hivyo kutatua changamoto ya ukosefu wa maji kwa wanafunzi katika shule hizo na kuzuia magonjwa mbaimbali ikiwemo ugonjwa wa matumbo.

Akizungumza mara baada ya kukagua miradi katika shule tatu za Unangwa,Msamala na Mkuzo,Mkurugenzi wa STOF nchini Marekani Teresa Nyirenda amewapongeza walimu na Kamati za Ujenzi kwa kusimamia vema utekelezaji wa miradi hiyo iliyofanikisha kupeleka maji katika shule tatu za msingi hivyo kutatua changamoto ya maji kwa wanafunzi katika shule hiyo.

“Unapoona mtoto hajakunywa maji tangu asubuhi,halafu chooni hakuna maji ni kitu ambacho kimenishitua hivyo sio STOF tu bali inatakiwa kuhamasisha hata wadau wengine kupita katika shule za msingi na kutatua changamoto mbalimbali zilizopo ikiwemo ukosefu wa maji nimejifunza kitu kikubwa sana kupitia ziara hii’’ Nyirenda,alisisitiza.

Ameahidi kuendelea kusaidia changamoto nyingine zikiwemo ukarabati wa vyoo vya wanafunzi katika shule ya msingi Unangwa ambapo amewapongeza Kamati ya ujenzi kwa kutumia fedha vizuri za kukarabati majengo ya shule hiyo ambayo yalikuwa chakavu.

Amesema Taasisi binafsi zinawajibu wa kuisaidia serikali katika kuhakikisha huduma muhimu zinawafikia wananchi kwa kuwa serikali pekee inasimamia miradi mingi na haiwezi kutekeleza huduma zote kwa asilimia 100 hivyo sekta binafsi zina mchango mkubwa.

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mkuzo Mwanaharusi Msomwa akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea, ameishukuru STOF kusaidia kuchimba kisima cha maji safi katika shule hiyo, hivyo ameomba ushirikiano kati ya STOF na Serikali uendelee katika masuala mbalimbali.

## NAMTUMBO ILIVYOBORESHA AFYA KWA WANANCHI



Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma ambayo ilianza kutoa huduma zake mwaka 2014 na kuanza huduma za upasuaji mwaka 2022, inaendelea kuwa kituo muhimu cha huduma za afya kwa wakazi wa wilaya hiyo.

Kulingana na taarifa ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Dr.Aron Hyera hadi sasa , hospitali hiyo inajivunia kuwa na jumla ya majengo 16 yaliyojengwa kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni tatu

“Majengo hayo yamekamilika na yanatumika, yakiwemo jengo la maabara, jengo la huduma za baba, mama na mtoto, jengo la macho, pamoja na jengo la afya ya kinywa”,alisema.

Amezitaja huduma zinazotolewa hospitalini hiyo kuwa ni pamoja na matibabu ya wagonjwa wa nje, huduma za maabara kwa vipimo mbalimbali, radiolojia, na kulaza wagonjwa wa aina mbalimbali, ikiwemo wanawake wanaojifungua na wanaohitaji upasuaji wa uzazi.

Aidha, hospitali hiyo inatoa huduma za kulaza wagonjwa wa kike, wa kiume, na watoto.

Hata hivyo amesema hivi karibuni, hospitali hiyo ilipokea kiasi cha shilingi milioni 575 kwa ajili ya kuboresha huduma zake. Kati ya fedha hizo, milioni 300 zimetengwa kwa ununuzi wa vifaa tiba.

Amesema zaidi ya milioni 200,zimetolewa kwa ujenzi wa miundombinu ya maji na ujenzi wa njia za kutembelea (walkways) ambazo zitaunganisha majengo yote ya hospitali hiyo.

Hatua hizi zinatarajiwa kuboresha zaidi huduma zinazotolewa hospitalini hapo na kuimarisha ustawi wa afya ya wakazi wa Wilaya ya Namtumbo.

## MBAMBABAY WAPONGEZA BARABARA ZA LAMI ZA MITAA



BAADHI ya wakazi wa wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma,wameipongeza Serikali kupitia Wakala wa Barabara za vijijini na mijini(TARURA) kwa kuboresha miundombinu na kujenga barabara za mitaa katika mji mdogo wa Mbambabay kwa kiwango cha lami.

Wamesema,ujenzi wa Barabara hizo umesaidia kurahisisha huduma ya usafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine, kuondoa adha ya vumbi kipindi cha kiangazi na matope kila inapofika msimu wa mvua pamoja na maeneo yao kupanda thamani ikilinganishwa na siku za nyuma.

Petro Zambala mkazi wa Mbambabay alisema,uamuzi wa Serikali ya awamu ya sita kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika mji huo utaharakisha

maendeleo na kuchochea kukua kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja na wilaya ya Nyasa.

Alisema,kabla ya barabara za lami baadhi ya huduma za kijamii zilipatikana kwa shida kwa sababu walishindwa kufika maeneo ya kutolea huduma hizo kwa wakati, jambo lililosababisha kuwa na maisha magumu.

Mkazi mwingine wa Mbambabay Nikaya Mbalale alisema,tangu Serikali ya awamu ya sita ilipoingia madarakani kuna mabadiliko makubwa katika mji huo hasa baada ya TARURA kupatiwa fedha nyingi ambazo zimewezesha kuboresha miundombinu ya barabara zake kwa lami, tofauti na siku za nyuma ambapo barabara nyingi za mitaa zilikuwa za vumbi.

Alisema,kuimarisha na kuboreshwa kwa barabara hizo zimehamasisha na kuwavutia watu wengi kwenda kuwekeza katika Mji wa Mbambabay ambao wananchi wake wanategemea shughuli za uvuvi na kilimo ili kuendesha maisha yao.

“ni jambo la faraja kwetu sisi wananchi Serikali yetu ya awamu ya sita kutujengea barabara za lami kwenye mitaa yetu,siku za nyuma tulipata shida kubwa kupitia kwenye maeneo haya kwenda kutafuta huduma za kijamii kwenye maeneo mengine”alisema Mbalale.

Aidha Mbalale,amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha zilizowezesha kukamilisha ujenzi wa mradi wa barabara ya Mbambabay- Mbinga yenye urefu wa kilometa 66 kwa kiwango cha lami.

Alisema,kukamilika kwa barabara hiyo kumesaidia kupunguza gharama za maisha na usafiri kwani hapo awali walikuwa wanalipa Sh.15,000 nauli ya kutoka Mbambabay hadi Mbinga lakini kwa sasa wanalipa Sh.9,000 hadi 10,000.

“kabla ya barabara ya lami ya Mbambabay-Mbinga,wilaya yetu ya Nyasa ilikuwa kama kisiwa kila inapofika msimu wa masika,barabara zilijifunga hivyo kuathiri shughuli za usafiri na usafirishaji wa mazao na bidhaa mbalimbali”alisema.

Alisema,Rais Samia Suluhu Hassan na Serikali yake imemaliza kero hiyo,sasa magari yanafika na kuondoka kwenye mji wa Mbambabay muda wowote na wananchi wanafanya shughuli zao za uzalishaji mali.




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura ( wa nne kutoka kulia) katika picha ya pamoja na maafisa kutoka Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi( wenye flana nyeupe) pamoja na maafisa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Maafisa hao walitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga tarehe 8 Januari 2024 kuhamasisha wanananchi kujitokeza katika zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura linalotarajia kuanza tarehe 12 hadi 18 januari 2024 katika Mkoa wa Ruvuma.



## RC RUVUMA AIPONGEZA SEKONDARI YA JENISTA MHAGAMA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ameipongeza Shule ya Sekondari ya Jenista Mhagama kwa usimamizi mzuri wa miradi ya shule na utunzaji wa mazingira.

Amewataka viongozi wa shule hiyo kukamilisha miradi iliyobaki, ikiwemo ujenzi wa bwalo la chakula kwa wanafunzi, kuongeza kiwango cha ufaulu, na kupanda miti ya matunda ili wanafunzi wanufaike nayo.

Akiwasilisha taarifa kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa shule hiyo, Mwalimu Felista Luambano, ameishukuru serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha sekta ya elimu.

Luambano amesema shule hiyo imepokea ufadhili wa shilingi 417,000,000 kutoka kampuni ya Barrick. Kati ya fedha hizo,kati ya fedha hizo shilingi . 17,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vyoo 10, shilingi 144,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba sita vya madarasa, na shilingi 256,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili.

# KANALI ABBAS AKAGUA MRADI WA UJENZI WA STENDI PARANGU



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amekagua mradi wa mabasi wa Kijiji cha Parangu, Halmashauri ya Wilaya ya Songea .

Akizungumza baada ya kukagua mradi huo Kanali Abbas amemuagiza mkandarasi kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati ili wananchi waanze kunufaika na huduma hiyo.

Amesisitiza ubora wa kazi na kuwapongeza wananchi wa Parangu kwa kushiriki katika ujenzi wa stendi kwa kuchimba msingi, mashimo ya vyoo, kusafisha eneo, kumwagilia maji, na kusongeza vifaa.

Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Parangu, Bw. Cosmas Mbute, akiwasilisha taarifa ya mradi huo, amesema kuwa ujenzi wa stendi ya mabasi ulianza tarehe 17 Desemba 2022 baada ya kupokea fedha za awamu ya kwanza kiasi cha Tsh. 202,833,871.43.

Amesema hadi Kufikia Mei 2023, waliomba fedha za awamu ya pili kutoka TASAF kiasi cha Tsh. 136,000,000 ambapo hadi sasa zimetumika zaidi ya shilingi milioni 315.

## MRADI UNAOKWENDA KUMALIZA KERO YA MAJI SONGEA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas , amefanya ukaguzi wa maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Miji 28 katika mji wa Songea.

Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 145.77 na unalenga kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa eneo hilo.

Kanali Abbas ametoa wito kwa Mkandarasi kuhakikisha kazi inaendelea bila kusimama.

Amehimiza kutumia vyanzo vingine vya fedha ili kuhakikisha ujenzi unasonga mbele kwa ufanisi.

“Mkandarasi anapaswa kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama kwa haraka,ni muhimu mradi huu ukamilike kwa ubora na ufanisi wa hali ya juu,” alisema Kanali Abbas

Akitoa taarifa kuhusu maendeleo ya mradi huo, Mhandisi Vicent Bahemana kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) amesema kuwa ujenzi huo unahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka Mto Njuga, uliopo kijiji cha Kikunja katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Amesema mradi huo unatarajia kuongeza uzalishaji wa maji hadi lita milioni 17 kwa siku, hatua hali ambayo itasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji katika mji wa Songea.

Mkurugenzi wa SOUWASA Mhandisi Patrick Kibasa amesema mradi huo huu unajumuisha ujenzi wa matenki matatu yenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 9 za maji pamoja na usambazaji wa bomba za maji umbali wa kilomita 34.7.

Mradi wa Miji 28 unatekelezwa na kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC). Hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia tano.



Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akizungumza baada ya kukagua mradi mkubwa wa maji katika eneo la Chandamali Manispaa ya Songea ,katikati ni Mkurugenzi wa SOUWASA Mhandisi Patrick Kibasa

Katika juhudi za kuboresha huduma za maji safi na usafi wa mazingira, serikali ya Tanzania imeanzisha Mradi wa Maji wa Miji 28, ambao unatekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mji wa Songea mkoani Ruvuma ni miongoni mwa miji inayonufaika na mradi huu, kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wake.

# RUVUMA WASHEREKEA KUZALIWA KWA RAIS KWA KUKATA KEKI




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas, ameongoza hafla ya kukata keki ya upendo kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Hafla hiyo imefanyika Januari 27, 2025, katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuhudhuriwa na viongozi wa serikali, wakuu wa wilaya, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), watumishi wa umma na wanahabari.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kanali Abbas alimpongeza Rais kwa kuongeza mwaka mwingine wa maisha na kumtakia afya njema, hekima na uvumilivu katika kulitumikia taifa. Pia, aliwashukuru watumishi wa umma na kuwasihi waendelee kufanya kazi kwa uadilifu na bidii.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma, Komred Oddo Mwisho, alisema chama kinaungana na viongozi wa mkoa kumpongeza Rais Samia, akisisitiza kuwa mchango wake kwa taifa unakumbukwa kila mwaka wa kuzaliwa kwake.

Hafla hiyo ilihitimishwa kwa dua na sala kwa ajili ya Rais pamoja na mshikamano wa viongozi katika kumtakia maisha marefu na mafanikio katika uongozi wake.

## MAHAKAMA KUU KANDA YA SONGEA YAZINDUA WIKI YA SHERIA




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amesema Mahakama ndio chombo pekee chenye wajibu wa kupiga vita dhuluma, uonevu, ukwepaji kodi, ubadhilifu wa mali za umma na matumizi mabaya ya mamlaka.

Ameyasema hayo wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria Nchini kwa Kanda ya Songea uliofanyika katika viwanja vya soko kuu la Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

"Ni dhahiri kuwa Mahakama ina kazi ya kupiga vita dhuluma, uonevu, ukwepaji kodi, ubadhilifu wa mali za umma, matumizi mabaya ya mamlaka au ofisi, kwa kuwa mahakama ndio chombo pekee chenye wajibu huo, nawaomba mfanye kazi zenu bila urasimu ama ukiritimba, na katika kufanya hivyo sio tu kwamba mtazidi kuheshimika bali pia mtapata thawabu mbele za Mwenyezi Mungu," alisema Kanali Ahmed.

Amewakumbusha wananchi kuwa chombo pekee cha kutatua mgogoro au shauri la aina yoyote ni Mahakama na sio sehemu nyingine, isipokuwa kwenye migogoro ambayo sheria imezipa taasisi zingine mamlaka ya kuisikiliza ili kuondoa migongano ya kimaslahi kati ya Mahakama na taasisi zingine.

Kwa upande wake Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Songea, Mhe. James Karayemaha, amesema kauli mbiu ya maadhimisho hayo mwaka 2025 inayosema

"TANZANIA YA 2050; Nafasi ya taasisi zinazosimamia haki madai katika kufikia malengo makuu ya dira ya taifa ya maendeleo" imebeba ujumbe mzito juu ya wajibu wa Mahakama na taasisi zinazoshughulikia haki madai katika kuhakikisha wanafikia malengo ya Dira ya mpango wa maendeleo ya Tanzania ya Mwaka 2050.

Amesema katika wiki hiyo ya sheria, Mahakama pamoja na wadau wa sheria watawaelimisha wananchi ndani ya mkoa wa Ruvuma juu ya shughuli za Mahakama kama chombo chenye mamlaka ya utoaji haki kikatiba na jinsi wadau na wananchi wanavyoshirikiana na chombo hicho katika utoaji haki, umuhimu wa amani, uzingatiaji wa sheria, kukwepa matumizi ya nguvu na kuchukua sheria mkononi ili kujenga misingi imara ya amani, mshikamano na umoja kwenye mkoa.

Ameongeza kuwa wananchi wataelimishwa kuhusu maboresho yanayoendelea ndani ya mahakama ikiwa ni pamoja na matumizi ya TEHAMA, ambapo watapewa elimu na wataalamu namna ya kupakua hukumu yake moja kwa moja kutoka mtandao unaoitwa TanzLII badala ya kusubiri hukumu iliyosomwa katika jengo la Mahakama Kuu, hivyo wananchi watumie wiki ya sheria kupata na kuongeza maarifa ya kisheria.



Kulia wa pili ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akizungumza kwenye uzinduzi wa  maadhimisho ya wiki ya sheria ngazi ya Mkoa wa Ruvuma yaliyofanyika katika viwanja vya soko kuu mjini Songea



Katika juhudi za kuboresha huduma za maji safi na usafi wa mazingira, serikali ya Tanzania imeanzisha Mradi wa Maji wa Miji 28, ambao unatekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mji wa Songea mkoani Ruvuma ni miongoni mwa miji inayonufaika na mradi huu, Mkurungezi wa Mamlaka ya Maji safi Songea (SOUWASA) Mhandisi Patrick Kibasa anasema Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 10 Machi 2023 kati ya Wizara ya Maji na China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kwa gharama ya TZS Bilioni 145.77.


**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**
**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**

**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**

**SIMU Nambari. 025-2602256/2602238**

**FAX Na. 2602144**

**E -MAIL:ras.ruvuma@tamisemi.go.tz**

**TOVUTI: www.ruvuma.go.tz**

**INSTAGRAM: rs ruvuma**

**FACEBOOK: rs ruvuma**

**YOUTUBE: rs ruvuma**